

JAMUHURI YA RWANDA



WIZARA YA MIUNDOMBINU  
E-mail : [info@mininfra.gov.rw](mailto:info@mininfra.gov.rw)  
P.O. Box 24 KIGALI

**TANGAZO**

Kulingana na makubaliano ya mukutano wa maraisi wa Jumuiya ya nchi za Afrika ya mashariki uliofanyika tarehe 12 Mei 2020 kwa njia ya video na mukutano wa Serikali ya Jamuhuri ya Rwanda na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanyika tarehe 15 Mei 2020;

Serikali ya jamuhuri ya Rwanda inapenda kufahamisha, wasafirishaaji wa bidhaa, waagizaji wa bidhaa toka nchi za nje na uma kwa ujumla maagizo ya utekelezaji wa haya yafuatayo:

1. Magari yote yanayoelekea Rwanda yatashusha mizigo sehemu iliondaliwa mipakani inayoitwa Kiyanzi(Kirehe) na Kagitumba (Nyagatare).
2. Kwa magari ambayo hayatashusha mizigo sehemu husika iliyotajwa hapo juu, yatafaurisha bidhaa hizo kwenye magari yalioandaliwa mipakani.
3. Kwa magari yaliobeba mizigo ambayo haiwezi kushushwa wala kufaurishwa sehemu husika iliyotajwa hapo juu, kutokana na aina ya bidhaa kama vile petrol na bidhaa zinazoweza kuharibika haraka kama inavyoonekana hapo nyuma, bidhaa hizo zitasindikizwa bila gharama yoyote mpaka zinapokwenda. Madereva watapumzika sehemu ilioandaliwa tu kwa ajili ya afya zaho.
4. Magari ya mizigo yataruhusiwa kutembea kati ya saa kumi na mbili (6h00)alfajiri mpaka sa kumi na mbili (6h00) jioni. Ili kufanikisha zoezi hili, wenye bidhaa wanapashwa kuanda jinsi ya kupakua na kupakia bidhaa zaho kabla madereva hawajatoka mipakani. Hii itasaidia kuepuka usambazaji wa virusi vya corona (COVID-19) kwa jamii nzima.
5. Wakati magari yaliosindikizwa yatakuwa hayajakamilisha ushushaji wa mizigo kwa muda uliopangwa, madereva watalala sehemu iliondaliwa na gharama za marazi zitalipwa na mwenye mizigo. Hii ni kwa usalama wa madereva na jamii nzima katika kuzuia wenezaji wa virusi vya corona (COVID-19)

6. Serikali ya Rwanda itaweka utaratibu wa upimaji wa madereva wote wanaopita Rwanda kwenda nje na wale waliobeba petroli na bidhaa zinazo haribika haraka zinazokuja Rwanda.
7. Bidha zote zinazoenda nje kupitia Rwanda zitasindikizwa kuanzia zinakoingilia hadi mpakani zinakovukia. Gharama za usindikizaji itakuwa juu ya serikali ya Rwanda.

**NB:**

- **Gharama za kupaki na kuhifadhi**

- i. Huduma zote za forodha, stoo za mizigo na huduma za utunzaji zinapatikana mipakani mizigo inakoingilia kwa usalama wa madereva, magari na bidhaa zao.
- ii. Kwa kuzingatia kuwa bidha zote zinapitia bandari kavu (Rwanda), mizigo yote inapashwa iondolewe ndani ya siku moja(1). Kinyume na hayo, gharama za kuhifadhi mizigo zitaongezeka faranga mbiri kwa kilo moja kila siku. (2 FRW/kilogram/siku).
- iii. Baada ya siku tatu bila kutoa mizigo(bidhaa), mizigo huo utasafirishwa kwenda stoo Kigali na gharama za usafirishaji na usalama wake (transport and insurance) zitakuwa juu ya mwenye mizigo.

- **Ulipaji wa forodha na mapata**

- i. Waagizaji wa mizigo wanaombwa kuhakikisha kuwa wasaidizi wao katika mambo ya forodha wameandaa malipo yote kabla ya mizigo kuondoka kupitia utalatibu wa *Single Customs Territory clearance framework*.
- ii. Ujazaji wa nyaraka zote za mizigo lazima zitolewe kwa njia za mitandao ya forodha. (*Rwanda electronic single window*)
- iii. Waagizaji wote wa bidhaa wanapashwa kutumia mufumo wa EBM version 2 (*electronic invoicing system*).

Imetolewa Kigali tarehe 19 Mei 2020



## **Orodha ya mizigo(bidhaa) itakayosindikizwa**

1. Bidhaa za Petroli
2. Bidhaa zinazoharibika haraka
3. Mzigo hatari ambayo haiwezi kuhifadhiwa na vitu vingine
4. Madawa na vifaa vyatibabu